

## **TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA UPIGAJI CHAPA KWENYE MIFUGO**

### **1.0 Utangulizi**

Utambuzi na Ufuatiliaji Mifugo ni mfumo unaoweza kuwa na alama na kumbukumbu ya mifugo kupitia usajili wa mifugo yenyewe, wamiliki wake, mahali ilipo na matukio muhimu kwenye uhai wa mifugo hiyo.

Utambuzi huu unaweza kuwa wa mnyama mmoja mmoja au wa kundi kwa maana ya alama moja kwa kundi la wanyama, mfano hapa Tanzania Utambuzi wa wanyama kwa kundi unafanyika kwa kila kijiji kuwa na alama moja ya chapa ya utambulisho wa kitaifa, na kwa Halmashauri ya wilaya ya Masasi utekelezaji wa zoezi hili limefanyika kwa kuweka alama moja ya chapa kwa kila kijiji. *(Angalia Kiambata A).*

### **2.0 Mafanikio ya utekelezaji wa zoezi**

Mfumo wa Utambuzi, Usajili na ufuatiliaji una lenga kudhibiti magonjwa ya mifugo, kudhibiti wizi wa mifugo, kuboresha kosaafu na mazao ya mifugo na nyama pia kuboresha soko la mifugo ndani na nje ya nchi sambamba na kusimamia usafirishaji wa mifugo na kusaidia kuweka majosho na malambo kwa ajili ya kuihudumia mifugo, pia Serikali kujua idadi ya mifugo iliyopo kwa lengo la kuirasimisha.

Halmashauri ilikuwa na lengo la kupiga Chapa Ng'ombe 6265 katika kata zake zote kulingana na zoezi la utambuzi lililo fanyika mwezi wa pili mwaka 2017, jumla ya Ng'ombe 9,274 wamepigwa chapa ambapo ni sawa na asilimia 148 ya utekelezaji. *Zoezi la uwekaji chapa ni zoezi endelevu kwa kuwa Ng'ombe wote walio pigwa chapa ni Ng'ombe wenye umri zaidi ya miezi sita na kuendelea, hivyo litakuwa linajirudia mara kwa mara ili kuendelea kutekeleza matakwa ya Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo. Na 12 ya mwaka 2010.*

### **3.0 Changamoto**

Kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa zoezi la chapa na kufanya utekelezaji kukwama kwa baadhi ya maeneo vijijini, ambapo miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na upatikanaji wa rasilimali fedha kwa wakati, utekelezaji katika ngazi ya kijiji ambapo ilitarajiwa kuwa kazi hii ingefanywa na mtaalamu wa ugani wa kijiji au kata kama suala la utekelezaji wa kawaida (*routine*) wakati wa utoaji huduma za ugani, kuwepo kwa mvua wakati wa utekelezaji wa zoezi hivyo kukwamisha utekelezaji, Wafugaji kutokuwa na maandalizi ya vibanio (*Animal crush*) na wengi wao kuwa kwenye shughuli za shamba wakati wa utekelezaji wa zoezi.

#### **4.0 Utatuzi wa Changamoto**

Changamoto zilizojitokeza zimetatuliwa kama ifuatavyo; Upatikanaji wa haraka wa rasilimali fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa (*Animal branding*) ambapo zoezi la ununuzi wa vifaa lilifanyika, kuwashirikisha wataalam waliopo ngazi za kata 10 kufanya zoezi katika kata zote na vijiji vyote, kuwahamasisha wafugaji ili waweze kuona umuhimu wa zoezi na kuandaa vibanio kwa ajili ya kurahisisha upigaji chapa.